

SHERIA ZA SHULE

1. Sheria za kiutu

- 1.1. Uwahi shuleni muda uliopangwa.
- 1.2. Uimbe kwa heshima, hali umesimama pamoja na kundi linalokuhusu, wimbo wa taifa unaotumiwa na shule kama sala ya pamoja kila siku kabla ya kuanza masomo.
- 1.3. Uwepo muda wote wa masomo na wa kazi ukifuata ratiba ya shule ndani na nje ya darasa ulilopangiwa.
- 1.4. Uheshimu picha takatifu, bendera na picha za viongozi wa nchi.
- 1.5. Uwe na tabia njema na utiifu kwa walimu, wafanyakazi na majirani wa shule, wanafunzi wenzako na binadamu yeyote.
- 1.6. Ukifikwiwa au kukutana na mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri usimame kumsalimia.
- 1.7. Ukiitwa na mwalimu yeyote umuitikie mara.
- 1.8. Uwe daima safi (mwili, nguo na vitu vyote unavyotumia).
- 1.9. Uwe na nywele fupi; usifuge ndevu.
- 1.10. Usijiremba kwa kutia nywele dawa, kujichora, kutia wanja n.k.
- 1.11. Usiache kucha ndefu wala kupaka rangi au hina.
- 1.12. Usivae kofia, jaketi, viatu vya ghorofa wala mapambo yoyote (herini, bangili, mikufu n.k.).
- 1.13. Uvae daima sare ukiwa shuleni (hata wakati wa likizo), ukitoka kwa shughuli za kishule, ukienda hospitalini, ukisafiri kufika shuleni au kurudi nyumbani, n.k.
- 1.14. Usionekane katika mazingira ya wasiwasi (klabu, kumbi za starehe, nyumba za wageni n.k.).
- 1.15. Usijihusishe na ulevi na uvutaji wa aina yoyote.
- 1.16. Usiwe na urafiki wa kimapenzi; hata hivyo ukipata mimba utakubaliwa likizo ya uzazi, usije ukaua mimba.
- 1.17. Ukae mahali pako katika darasa ulilopangiwa, pasipo kuhamahama wala kuchanganyikana na jinsia nyingine.
- 1.18. Ufanye kwa bidii kazi za aina zote, ukishirikiana na wenzako katika usafi na utunzaji wa mazingira.
- 1.19. Ulinde mali yako binafsi na ya shule (majengo, madawati, vitabu na vifaa vingine utakavyopewa).
- 1.20. Usitoe dawati nje ya jengo lake pasipo agizo au ruhusa.
- 1.21. Utambue ni marufuku kuiba, kugombana, kupigana, kutumia lugha chafu, kuchonganisha, kuchochea vurugu na kufanya mgomo.
- 1.22. Usitembelee nyumba za walimu na wafanyakazi wengine wala bweni la jinsia tofauti.
- 1.23. Usitoroke shule, bali utoe taarifa kama utashindwa kuhudhuria masomo.
- 1.24. Usilete shuleni simu, redio n.k. la sivyo utafukuzwa mara moja.
- 1.25. Uombe ruhusa ukitaka kuleta shuleni magazeti, majarida, vitini, vitabu n.k.
- 1.26. Ukubali mamlaka ya wanafunzi viongozi katika kushauri, kuonya na hata kuadhibu kabla tatizo lako halijaufikia utawala wa shule.
- 1.27. Usikatae adhabu.

2. Sheria za kitaaluma

- 2.1. Uwe msikivu na mtekelezaji wa maagizo na mashauri ya walimu.
- 2.2. Ukamilishe kazi zote zinazotolewa na walimu kwa wakati unaotakiwa.
- 2.3. Uwe mtulivu muda wote darasani, mwalimu awepe au asiwepo vilevile.
- 2.4. Ushirikiane vema na walimu pamoja na wanafunzi wenzako ili kupata msaada wa kitaaluma.
- 2.5. Ujitahidi kufanya vizuri mitihani ya mara kwa mara, usije ukaondolewa shuleni kwa kutoifanya mara tatu mfululizo (hata kama umeruhusiwa kwa shida maalumu) au kwa kutofikia mara mbili mfululizo wastani wa alama 45 kwa jumla ya masomo yote, na wa alama 21 kwa somo la hisabati.
- 2.6. Utambue ni kosa kubwa kuibia, kusaidiwa au kusaidia katika mitihani wowote.

3. Sheria za nyongeza kwa wanaokaa bweni (hata la nje)

- 3.1. Uvae sare ya bweni muda wote, bila ya kuichanganya na vazi lingine wala urembo wowote.
- 3.2. Uombe ruhusa ukihataji kurudi bweni wakati wa vipindi darasani.
- 3.3. Uzingatie muda wa chakula kwa sababu huruhusiwi kukipeleka bweni.
- 3.4. Usiwasiliane na mtu yeyote bila ya mkuu wa bweni kujua.
- 3.5. Usimpokee mgeni yeyote tofauti na walioandikwa na mzazi, wala nje ya siku za kutembelewa, tena upate kwanza ruhusa ya mkuu wa bweni na usimuingize bweni.
- 3.6. Usiende nje bila ya ruhusa maalumu; ukienda kwenye ibada uvae sare na kurudi shuleni mara, bila ya kupitia sehemu nyingine.

4. Adhabu

- 4.1. Kwa kosa la kukwepa mitihani wa somo lolote, na vilevile la kuibia, kusaidiwa au kusaidia wakati wa kuufanya, utandikiwa alama sifuri (0%) katika matokeo yako.
- 4.2. Kwa baadhi ya makosa utapewa kwanza maonyo mawili, ambayo yataandamana na adhabu shuleni na kudai uandike barua ya kukiri kosa na kuahidi hutalirudia.
- 4.3. Kwa makosa makubwa zaidi hutapewa maonyo, bali utasimamishwa kwa siku au wiki kadhaa, kama si kufukuzwa shule.
- 4.4. Ukifukuzwa bweni hutaruhusiwa kuendelea na masomo kama mwanafunzi wa kutwa.
- 4.4. Ukipoteza au kuharibu kitabu au kitu chochote cha shule utatakiwa kununua kipya na kurejesha, la sivyo hutarudishiwa fedha za tahadhari.

4.5. Vitu visivyotakiwa shuleni vikinyang'anywa na uongozi hutarudishiwa.